JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Nyamagana" Posta Road,
S.L.P. 2599,
MWANZA,
Barua Pepe: rbcmwanza@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

MWANZA – JULAI 8, 2020

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU MISUNGWI – MWANZA YAOKOA SHILINGI 18,277,000/=

1.0 UTANGULIZI:

KUREJESHWA KWA SH. 10,000,000/= ZILIZOCHUKULIWA KWA UTARATIBU WA MIKOPO INAYOUMIZA WAKOPAJI

Mnamo tarehe 21.05.2020 Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza ilipokea taarifa kutoka kwa Mwalimu Mstaafu aitwaye AUGUSTINE JOSEPH NGOWI kuwa amedhulumiwa mafao yake ya kustaafu na mtu aitwaye EMMANUEL DANIEL CHACHA Mkazi wa Misungwi - Mwanza.

Taarifa ilidai kwamba mwalimu huyo baada ya kustaafu na kulipwa mafao yake ya zaidi ya sh milioni 95 - jumla ya shs milioni 14,900,000/= zilichukuliwa kwenye akaunti yake na mlalamikiwa kwa njia isiyo halali.

2.0 UCHUNGUZI

Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza ulianzishwa na kubaini yafuatayo:

- Mwl Augustine Joseph Ngowi (62) alikuwa mtumishi wa umma-Mwalimu Mkuu katika Shule ya Msingi Mwanangwa iliyopo wilayani Misungwi Mkoa wa Mwanza.

- Mwalimu Ngowi alistaafu kwa lazima mnamo tarehe 12.12.2018 na kulipwa mafao yake ya kustaafu na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii – NSSF (Kwa sasa PSSSF) tarehe 17.04.2019.

- Uchunguzi umebaini pia kwamba Mwl Augustine Joseph Ngowi alikopa fedha kwa EMMANUEL DANIEL CHACHA (32) kiasi cha Sh 3,490,000/ kwa kipindi cha kuanzia Novemba 2018 hadi April 2019 ambapo walikubaliana kulipana mkopo huo kwa riba ya 20% kwa kila mwezi.

- Fedha aliyokopeshwa alipewa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza alipewa sh 390,000/= CASH mwezi Novemba 2018, aidha tarehe 24 Disemba 2018 aliwekewa sh 1,000,000/- kwenye akaunti yake ya benki ya NMB Akaunti namba 31308000647, Tarehe 13 Februari 2019, alikopa sh 600,000/ ziliingizwa kwenye akaunti yake, na tarehe 11 Machi, 2019 alikopa sh 300,000/ nazo ziliingizwa kwenye akaunti yake na mwisho ni tarehe 10 April 2019 alikopa sh 1,200,000/ nazo ziliingizwa kwenye akaunti yake, hivyo jumla ya fedha yote aliyokopa ni sh 3,490,000/-. Wakati wanakopeshana walisainishana mkataba ambao hata hivyo mkataba huo ulichanwa baada ya mlalamikiwa kuchukua fedha kiasi cha sh 14,900,000/- baada ya mafao ya mstaafu huyo kutoka.

- Mlalamikiwa baada ya kutoa mkopo alishikilia kadi ya benki ya mkopaji pamoja na namba ya siri ambapo alikuwa akitumia kadi hiyo kuangalia salio mara kwa mara kwenye akaunti ya mkopaji ya Mwl Augustine Joseph Ngowi.

- Mnamo tarehe 17.04.2019 Mwl Augustine Joseph Ngowi alipokea mafao yake ya kustaafu ambapo fedha ziliwekwa kwenye akaunti yake.

- Tarehe 23 April 2019 Emmanuel Daniel Chacha alikwenda benki ya NMB Misungwi na kuangalia salio kwenye akaunti ya Mwl. Augustine Joseph Ngowi ambapo alibaini ya kuwa tayari mafao ya mwalimu huyo yamekwisha pokelewa kwenye akaunti hiyo.

- Baada ya kukuta kuna fedha alimjulisha mwalimu Augustine Joseph Ngowi ambapo alimtaka afike Misungwi ili aweze kutoa fedha na kulipa mkopo huo. Tarehe 24.4.2019 mwalimu Augustine Joseph Ngowi alifika kwa Emmanuel Daniel Chacha ambapo mkopeshaji huyo alimwacha mwalimu huyo nyumbani na kwenda kwa wakala wa NMB na kuhamisha kiasi cha Tsh 14,900,000/-.

- Kati ya fedha hizo kiasi cha Sh. 14,000,000/- kiliwekwa kwenye akaunti ya Hamis Daniel Marwa akaunti namba 50710008439 ya NMB ambaye ni mdogo wake mkopeshaji, na Tsh 900,000/- aliziweka kwenye akaunti yake yeye mwenyewe Emmanuel Daniel Chacha akaunti namba 313110009120 NMB.

Baada ya uchunguzi wa kina kufanyika na kubaini ukweli wa malalamiko haya, Bw Emmanuel Daniel Chacha alikiri kuchukua fedha hizo na akaagizwa kuzirejesha mara moja.

Tayari fedha hizo kiasi cha sh 10,000,000/= zimerejeshwa ili akabidhiwe Mwl Augustine Joseph Ngowi.

WITO:

Ninawataka wakopeshaji wote katika Wilaya hii ya Misungwi kufuata taratibu na sheria ikiwemo kujisajili katika vyombo husika vya Serikali na kufanya biashara hiyo wakiwa na leseni halali huku wakilipa mapato ya Serikali vinginevyo Serikali hususani TAKUKURU itawachukulia hatua za kisheria.

Aidha ni vema wakopaji wote hususani wastaafu wanaosubiri kulipwa mafao yao, wote wakaepuka mikopo umiza yenye riba kubwa.

2.0 KUREJESHWA KWA SHS 1,227,000/= KUTOKANA NA MRADI WA UJENZI WA MABOMA SHULE YA SEKONDARI IGOKELO.

2.1 UTANGULIZI:

Ofisi ya TAKUKURU wilaya ya misungwi mkoani Mwanza kupitia moja ya majukumu yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ilifanikiwa kuokoa kiasi cha sh 1,227,000/= katika mradi wa ukamilishaji wa maboma ya Shule ya Sekondari IGOKELO. Katika mradi huo kila kijiji kilitakiwa kujenga boma lake na mradi huo uliojumuisha jumla ya vijiji sita.

2.2 UCHUNGUZI:

Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya Misungwi ulibaini kwamba:

- Kijiji cha Busolwa kilishindwa kukamilisha boma lake kutokana na usimamizi mbovu wa fedha zilizokusanywa.

- Jumla ya fedha zilizokusanywa katika kijiji cha Busolwa ni sh **4,160,500** na zilizotumika zilikuwa sh 2,933,500 na hivyo kufanya jumla ya fedha zilizopotea kuwa sh **1,227,000/=**

- Viongozi wa vijiji na kata ndiyo waliokuwa wanahusika katika usimamizi wa fedha zote zilizokusanywa kutoka kwa wananchi na wao ndiyo waliofanya matumizi mabaya ya hizo fedha, hivyo ofisi ya TAKUKURU (W) Misungwi iliwataka viongozi wote waliohusika kuzirejesha fedha hizo **sh 1,227,000/=** mara moja katika ofisi ya TAKUKURU wilaya ya Misungwi na tayari fedha hizo zimerejeshwa ili zipelekwe katika ujenzi wa mradi husika ambao ni kumalizia darasa lililotakiwa kujengwa na kijiji cha Busolwa.

3.0 KUREJESHWA KWA TSHS 7,050,000/= ZA MAKUSANYO YA MAPATO KWA KUTUMIA MASHINE ZA KI ELEKTRONIKI (POS) KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

3.1 UTANGULIZI:

Ofisi ya TAKUKURU (W) Misungwi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeokoa kiasi cha fedha sh **7,050,000/=** zilizokusanywa kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato lakini hazikuwasilishwa Benki kwenye akaunti ya kukusanyia mapato ndani ya Halmashauri.

3.2 UCHUNGUZI:

Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza umebaini kwamba:

- Fedha hizo walikuwa wanadaiwa wakusanya mapato waliokuwa wanakusanya mapato kwa kutumia Point of sale (POS) mashine.

- Mapato yaliyokuwa yanakusanywa ni ya kipindi cha mwaka 2018/2019 na walishindwa kuwasilisha Benki katika akaunti ya Halmashauri ya wilaya ya Misungwi.

- Ofisi ya TAKUKURU (W) Misungwi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi iliwatafuta wadaiwa wote walioshindwa kuwasilisha fedha Benki na kuwataka kurejesha fedha hizo zenye jumla ya Tsh **7,050,000/=.**

- **Tayari kiasi cha shilingi 725,000/= zimeshawekwa Benk na kiasi cha sh 6,325,000/=** leo zinakabidhiwa ili zipelekwe Benki katika akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

WITO:
Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Misungwi kwa kipindi cha mwezi Juni 2020 imeokoa jumla ya kiasi cha shilingi **18,277,000/=** ambazo zote leo zimekabidhiwa kwa wahusika mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Misungwi.

EMMA MWASYOGE

MKUU WA TAKUKURU WILAYA YA MISUNGWI

KNY: MKUU WA TAKUKURU (M) MWANZA